

Orodha Hakikishi ya Kabla ya Chanjo za COVID-19



Kwa wapokeaji wa chanjo:

Maswali yafuatayo yatatusaidia kujua ikiwa kuna sababu yoyote hupaswi kupokea chanjo ya COVID-19 leo. **Endapo utajibu "ndiyo" kwa swali lolote, haimaanishi kuwa hupaswi kupata chanjo.** Inamaanisha tu kuwa maswali ya ziada yanaweza kuulizwa. Ikiwa swali halieleweki, tafadhali muulize mtoa huduma wako wa afya afafanue zaidi.

Jina _____

Umri _____

	Ndiyo	Hapana	Sijui
1. Je, unahisi kuugua leo?	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
2. Je, umewahi kupokea dozi ya chanjo ya COVID-19?	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
<ul style="list-style-type: none"> Ikiwa ndiyo, umepokea aina gani ya chanjo? <ul style="list-style-type: none"> <input type="checkbox"/> Pfizer <input type="checkbox"/> Moderna <input type="checkbox"/> Janssen (Johnson & Johnson) <input type="checkbox"/> Aina Nyingine _____ Je, umekuja na kadi au nyaraka nyingine ya kumbukumbu zako za chanjo? (ndiyo/hapana) 	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
3. Je, umewahi kupata athari ya mzio kwa: (Hii ni pamoja na athari kali za mzio [kwa mfano, mzio mkali na hatarishi kwa maisha ya mtu] ambayo ilihitaji matibabu kwa kutumia epinephrine au EpiPen® au ambayo ilikuhitaji uende hospitalini. Inajumuisha pia athari ya mzio ambayo ilisababisha mabaka kwenye ngozi, uvimbe, au matatizo ya kupumua, ikiwa ni pamoja na kutoa sauti ya winja/mluzi mtu anapopumua.)			
<ul style="list-style-type: none"> Kijenzi cha chanjo ya COVID-19, ikiwa ni pamoja na moja ya yafuatayo: <ul style="list-style-type: none"> Polyethylene glycol (PEG), ambayo hupatikana katika baadhi ya dawa, kama vile dawa za kuhara na maandalizi ya taratibu za uchunguzi wa utumbo mpana Polysorbate, ambayo hupatikana katika baadhi ya chanjo, tembe zilizowekwa utando, na steroidi za kuchomwa kwenye mishipa Dozi ya awali ya chanjo ya COVID-19 	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
4. Je, umewahi kupata athari ya mzio kwa chanjo nyingine (mbali na chanjo ya COVID-19) au dawa kwa kudungwa sindano? (Hii ni pamoja na athari kali za mzio [kwa mfano, mzio mkali na hatarishi kwa maisha ya mtu] ambayo ilihitaji matibabu kwa kutumia epinephrine au EpiPen® au ambayo ilikuhitaji uende hospitalini. Inajumuisha pia athari ya mzio ambayo ilisababisha mabaka kwenye ngozi, uvimbe, au matatizo ya kupumua, ikiwa ni pamoja na kutoa sauti ya winja/mluzi mtu anapopumua.)	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
5. Chagua zote zinazohusika kwako:			
<input type="checkbox"/> Mimi ni mwanamke wa kati ya umri wa miaka 18 na 49			
<input type="checkbox"/> Nimekuwa na athari kali ya mzio kwa kitu kingine mbali na chanjo au tiba ya sindano kama vile mizio ya vyakula, mnyama kipenzi, sumu, mazingira au dawa za kumeza			
<input type="checkbox"/> Nilikuwa na COVID-19 na nilitibiwa kwa kingamwili za protini zinazotengenezwa katika maabara (monokloni) au seramu ya damu kutoka kwa mtu aliyepata ahueni			
<input type="checkbox"/> Nimegundulika kuwa nina Ugonjwa wa Kuvimba Viungo Vingi (MIS-C au MIS-A) baada ya maambukizi ya COVID-19			
<input type="checkbox"/> Nina kinga dhaifu (yaani, maambukizi ya VVU, saratani)			
<input type="checkbox"/> Ninatumia dawa au tiba zinazofubaza ukosefu kinga			
<input type="checkbox"/> Nina matatizo ya kuvuja damu			
<input type="checkbox"/> Ninatumia dawa za kuzuia kuganda kwa damu			
<input type="checkbox"/> Nina historia ya kuwa na idadi ndogo ya chembechembe za damu inayosababishwa na heparini (HIT)			
<input type="checkbox"/> Kwa sasa mimi ni mjamzito au ninanyonyesha			
<input type="checkbox"/> Nimedungwa vijaza ngozi			

Fomu imekaguliwa na _____

Tarehe _____

Ukurasa huu uliachwa wazi makusudi.

Orodha Hakikishi ya Kabla ya Chanjo za COVID-19

Maelezo kwa Wataalamu wa Huduma ya Afya



Kwa maelezo zaidi kuhusu mwongozo wa kimatibabu wa chanjo ya COVID-19, angalia

<https://www.cdc.gov/vaccines/covid-19/info-by-product/clinical-considerations.html>.

Kwa maelezo zaidi kuhusu Kamati ya Ushauri wa Desturi za Chanjo Miongozo ya Jumla ya Desturi Bora Zaidi za Chanjo, angalia <https://www.cdc.gov/vaccines/hcp/acip-recs/general-recs/index.html>.

Chanjo za COVID-19 zimeidhinishwa kwa makundi ya umri tofauti na hudungwa ndani ya misuli kama mfululizo wa dozi mbili au dozi moja.

AINA YA CHANJO	MAKUNDI KWA UMRI YALIYODHINISHWA	MFULULIZO	KIPINDI
Chanjo ya COVID-19 ya Pfizer-BioNTech	Umri wa miaka 12 na zaidi	Dozi 2	Siku 21
Chanjo ya COVID-19 ya Moderna	Umri wa miaka 18 na zaidi	Dozi 2	Siku 28
Chanjo ya COVID-19 ya Janssen (Johnson & Johnson)	Umri wa miaka 18 na zaidi	Dozi moja	HAIHUSIKI

Mtu yeyote nje ya makundi kwa umri yaliyodhinishwa kwa aina fulani hapaswi kupokea chanjo hiyo.

Muda wa Uchunguzi Baada ya Chanjo kwa Watu Wasiopata Athari ya Chanjo ya COVID-19

▪ Dakika 30:

- Historia ya athari ya mzio wa ukali wowote baada ya muda mfupi kwa chanjo au tiba ya sindano
- Hali inayozuia usipate aina tofauti ya chanjo ya COVID-19 (kwa mfano, watu walio na athari kwa chanjo za mRNA ambao hupokea Janssen (Chanjo ya COVID-19 ya Johnson & Johnson)
- Historia ya mzio mkali na hatarishi kwa maisha ya mtu kwa sababu yoyote

▪ Dakika 15:

- Watu wengine wote

Kupewa chanjo za COVID-19 pamoja na chanjo zingine

Chanjo za COVID-19 na chanjo zingine **zinaweza kutolewa bila kuzingatia wakati**. Hii inajumuisha utoaji wa pamoja wa chanjo za COVID-19 pamoja na chanjo zingine wakati wa ziara moja. Chanjo zingine pia zinaweza kutolewa wakati wowote kabla au baada ya chanjo ya COVID-19.

1. Je, unahisi kuugua leo?

Ingawa hakuna ushahidi kuwa ugonjwa mkali unapunguza ufanisi wa chanjo au huongeza athari mbaya, kwa tahadhari, **chelewesha kuwapa chanjo wagonjwa wenye ugonjwa wa wastani au mkali hadi maradhi yapate nafuu.**

Ahirisha chanjo kwa watu walio na maambukizi ya sasa ya SARS-CoV-2 hadi mtu huyo apone kutokana na ugonjwa mkali na akamilishe kujitenga. Pendekezo hili linatumika bila kujali ikiwa

maambukizi ya SARS-CoV-2 yalitokea kabla ya mpokeaji kupata dozi ya kwanza au kipindi baina ya dozi na dozi, kwa chanjo ya dozi mbili. Upimaji wa virusi au serolojia ili kutathmini maambukizi ya sasa au ya awali kwa madhumuni tu ya kufanya uamuzi wa chanjo haupendekezwi.

Watu walio na maradhi yasiyo makali wanaweza kupewa chanjo. Usizuie kutoa chanjo ikiwa mtu anatumia viua vijasumu.

Orodha Hakikishi ya Kabla ya Chanjo za COVID-19

Maelezo kwa Wataalamu wa Huduma ya Afya



2. Je, umewahi kupokea dozi ya chanjo ya COVID-19?

Chanjo za COVID-19 haziwezi kubadilishwa.

Kwa chanjo zinazotolewa kwa dozi mbili, angalia kumbukumbu za matibabu, mifumo ya maelezo ya chanjo, na kadi za kumbukumbu za chanjo ili zikusaidie kubaini aina ya chanjo ya kwanza iliyopokelewa. Ikiwa aina ya chanjo inayotumiwa kwa dozi ya kwanza haiwezi kubainishwa au haipatikani tena, chanjo yoyote inayopatikana ya mRNA

inaweza kutolewa (tenganisha dozi kwa angalau siku 28). Ikiwa dozi mbili za chanjo tofauti za mRNA za COVID-19 zinatolewa bila kukusudia, hakuna dozi za ziada za chanjo hiyo zinapendekezwa.

Watu ambao walipokea chanjo ya majaribio wanapaswa kushauriana na wadhamini wa jaribio ili kubaini ikiwa inawezekana kupokea dozi za ziada.

Kwa watu ambao walipokea chanjo ya COVID-19 nje ya Marekani:

- Watu ambao walipokea dozi zote zilizopendekezwa za chanjo ya COVID-19 iliyoidhinishwa na FDA hawahitaji dozi zozote za ziada. Watu ambao walipokea dozi ya kwanza cha chanjo ya COVID-19 iliyoidhinishwa na FDA ambayo inahitaji dozi mbili **hawahitaji** kuanza tena mfululizo wa chanjo wakiwa Marekani lakini wanapaswa kupokea dozi ya pili karibu na wakati unaopendekezwa iwezekanavyo.
- Watu ambao wamepokea dozi zote zilizopendekezwa za chanjo ya COVID-19 iliyoorodheshwa kwa matumizi ya dharura na WHO **hawahitaji** dozi yoyote ya ziada ya chanjo ya COVID-19 iliyoidhinishwa na FDA. Angalia Mazingatio ya Kimatibabu ya Muda kwa Matumizi ya Chanjo za COVID-19 Zilizoidhinishwa Hivi sasa nchini Marekani (<https://www.cdc.gov/vaccines/covid-19/info-by-product/clinical-considerations.html>) kwa orodha ya chanjo za WHO za matumizi ya dharura.
- Watu ambao hawajapata dozi zote zilizopendekezwa za chanjo ya COVID-19 iliyoorodheshwa kwa matumizi ya dharura na WHO wanaweza kupewa mfululizo kamili wa chanjo iliyoidhinishwa na FDA ya COVID-19. Subiri angalau siku 28 baada ya dozi ya mwisho ya chanjo ambayo haijaidhinishwa na FDA kabla ya kutoa chanjo ya COVID-19 iliyoidhinishwa na FDA.
- Watu ambao walipokea baadhi ya dozi zote au baadhi ya dozi zilizopendekezwa za chanjo ya COVID-19 ambazo hazijaorodheshwa kwa matumizi ya dharura na WHO na ambazo haijaidhinishwa na FDA wanaweza kupewa mfululizo kamili wa chanjo ya COVID-19 iliyoidhinishwa na FDA. Subiri angalau siku 28 baada ya dozi ya mwisho ya chanjo ambayo haijaidhinishwa kabla ya kutoa chanjo ya COVID-19 iliyoidhinishwa na FDA.

3. Je, umewahi kupata athari ya mzio kwa:

- Kijenzi chochote cha chanjo ya COVID-19, ikiwa ni pamoja na:
 - Polyethylene glycol (PEG), ambayo hupatikana katika baadhi ya dawa, kama vile dawa za kuhara na maandalizi ya taratibu za uchunguzi wa utumbo mpana
 - Polysorbate, ambayo hupatikana katika baadhi ya chanjo, tembe zilizowekwa utando, na steroidi za kupitishwa mishipani
- Dozi ya awali ya chanjo ya COVID-19

Watu wanaopata athari ya mzio baada ya muda mfupi* kwa dozi ya awali ya chanjo ya COVID-19 au mzio unaojulikana (uliotambuliwa) kwa kijenzi cha chanjo wana hali inayowazuia wasipate chanjo.

Watu walio na hali inayowazuia wasipate chanjo ya mRNA ya COVID-19 hawapaswi kupokea dozi ya chanjo yoyote ya mRNA (Pfizer-BioNTech au Moderna). Watu walio na hali inayowazuia wasipate chanjo ya mRNA COVID-19 (ikiwa ni pamoja na mzio unaojulikana [uliotambuliwa] kwa PEG†) wana tahadhari kwa Chanjo ya Janssen ya COVID-19.

Watu walio na hali inayowazuia wasipate Chanjo ya Janssen ya COVID-19 (ikiwa ni pamoja na mzio unaojulikana [uliotambuliwa] kwa polysorbate*) wana tahadhari kwa chanjo za mRNA za COVID-19.

Watu walio na historia ya kupata athari ya mzio baada ya muda mfupi kwa chanjo au tiba ya sindano ambayo inajumuisha vijenzi vingi, kimoja au zaidi ya hivyo ni kijenzi cha chanjo ya COVID-19, wana tahadhari ya kuchanjwa na chanjo hiyo ya COVID-19, hata kama haijulikani ni kijenzi gani kinachosababisha athari ya mzio.

*Wakati wapokeaji wa chanjo wanapotoa taarifa ya historia ya athari ya mzio ya baada ya muda mfupi, watoa huduma wanapaswa kujaribu kubaini endapo athari zinazotarifiwa kufuatia chanjo zinalingana na athari za mzio za baada ya muda mfupi dhidi ya aina zingine za athari zinazoonekana sana kufuatia chanjo, kama vile athari ya kupoteza fahamu (vasovagal) au athari ya baada ya chanjo (ambazo sio hali zinazozuia kupokea dozi ya pili ya chanjo ya mRNA ya COVID-19).

†Polyethylene glycol (PEG) ni kiambato katika chanjo zote za mRNA za COVID-19, na polysorbate 80 ni kiambato katika Chanjo ya Janssen ya COVID-19. Kwa sababu PEG na polysorbate zinahusiana kimuundo, mmitikio wa kiwango cha juu wa protini tofauti kati ya michanganyiko hii unaweza kutokea.

Orodha Hakikishi ya Kabla ya Chanjo za COVID-19

Maelezo kwa Wataalamu wa Huduma ya Afya



Vijenzi vya Chanjo ya COVID-19*

Maelezo	Chanjo ya mRNA ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19	Chanjo ya mRNA ya Moderna ya COVID-19	Chanjo ya Janssen ya COVID-19
Viambato hai	mRNA ambayo baadhi ya nukleosidi zimebadilishwa inayobainisha glikoprotini ya spike (S) ya virusi vya SARS-CoV-2	mRNA ambayo baadhi ya nukleosidi zimebadilishwa inayobainisha glikoprotini ya spike (S) ya virusi vya SARS-CoV-2	Virusi Salama; Virusi salama vya mchanganyiko kutoka vyanzo tofauti, visivyoweza kurudufu vya Ad26, vinavyobainisha aina thabiti ya protini ya Spike (S) ya SARS-CoV-2
Viambato tulivu	2[(polyethylene glycol {PEG}- 2000)-N, N-ditetradecylacetamide	PEG2000-DMG: 1,2-dimyristoyl-rac-glycerol, methoxypolyethylene glycol	Polysorbate-80
	1,2-distearoyl-sn-glycero-3-phosphocholine	1,2-distearoyl-sn-glycero-3-phosphocholine	2-hydroxypropyl-β-cyclodextrin (HBCD)
	Lehemu	Lehemu	Citric acid monohydrate
	(4-hydroxybutyl)azanediylbis(hexane-6,1-diyl)bis(2-hexyldecanoate)	SM-102: heptadecan-9-yl 8-((2-hydroxyethyl) (6-oxo-6-(undecyloxy) hexyl) amino) octanoate	Trisodium citrate dihydrate
	Chumvi	Tromethamine	Chumvi
	Monobasic potassium phosphate	Tromethamine hydrochloride	Ethani
	Chumvi ya potasiamu	Tindikali itokanayo na matunda	
	Dibasic sodium phosphate dihydrate	Chumvichumvi ya sodiamu	
Sukari ya muwa na kiazia	Sukari ya muwa na kiazia		

*Hakuna chanjo inayojumuisha mayai, jelatini, ulimbo wa mpira au dawa za kuzuia kuoza.

Sifa zinazowezekana za athari ya mzio, athari za kupoteza fahamu, na athari za chanjo kufuatia chanjo ya COVID-19

Kwa wagonjwa ambao hupata dalili baada ya chanjo, hatua ya kubaini chanzo cha magonjwa (ikiwa ni pamoja na athari ya mzio, athari ya kupoteza fahamu, au athari za chanjo) ni muhimu ili kubaini ikiwa mtu anaweza kupata dozi za ziada za chanjo (ikiwa ni pamoja na dozi ya 2 ya chanjo ya mRNA ya COVID-19). Jedwali lifuatalo la ishara na dalili

linanua kutumika kama nyenzo lakini halijumuishi maelezo yote, na huenda wagonjwa wasipate dalili au ishara zote. Watoa huduma wanapaswa kutumia uamuzi wao wa kimatibabu wanapochunguza wagonjwa ili kubaini utambuzi na usimamizi unaofaa.

Sifa	Athari za mzio za baada ya muda mfupi (ikiwa ni pamoja na mzio mkali na hatarishi kwa maisha ya mtu)	Athari za kupoteza fahamu	Athari mbaya za chanjo (katika eneo la kudungwa na la kimfumo)
Muda baada ya chanjo	Nyingi hutokea ndani ya dakika 15-30 baada ya chanjo	Nyingi hutokea ndani ya dakika 15	Wastani wa siku 1 hadi 3 baada ya chanjo (huku nyingi zikitokea siku inayofuata baada ya kupata chanjo)

ISHARA NA DALILI

Sifa	Athari za mzio za baada ya muda mfupi (ikiwa ni pamoja na mzio mkali na hatarishi kwa maisha ya mtu)	Athari za kupoteza fahamu	Athari mbaya za chanjo (katika eneo la kudungwa na la kimfumo)
Kwa mwili mzima	Hisia ya kutaka kufa	Kuhisi joto au baridi	Homa, ubaridi, uchovu
Kwenye ngozi	Dalili za ngozi zinazopatikana katika ~90% ya watu walio na mzio mkali na hatarishi kwa maisha ya mtu, ikiwa ni pamoja na mwasho(pruritus), vipele(urticaria), wekundu(flushing), uvimbe chini ya ngozi (angioedema)	Weupe (Pallor), utokwaji jasho nyingi (diaphoresis), ngozi nyevu/yenye jasho, hisia ya joto kwenye uso	Maumivu, wekundu (erythema) au uvimbe kwenye eneo lililodungwa sindano, kuvimba kwa tezi za limfu (lymphadenopathy) katika mkono uliodungwa chanjo
Kwenye mfumo wa Neva hasa kichwani	Kuchanganyikiwa, kuvurugika mawazo, kizunguzungu, kuhisi kuzirai, udhaifu, kupoteza fahamu	Kizunguzungu, kuhisi kuzirai, kupoteza fahamu (mara nyingi baada ya dalili za mapema kwa sekunde au dakika chache), udhaifu, mabadiliko katika uwezo kwa kuona (kama vile kumwekamweka kwa taa, kuona tu sehemu kwa wembamba), mabadiliko katika uwezo wa kusikia	Maumivu ya kichwa

Orodha Hakikishi ya Kabla ya Chanjo za COVID-19

Maelezo kwa Wataalamu wa Huduma ya Afya



Sifa	Athari za mzio za baada ya muda mfupi (ikiwa ni pamoja na mzio mkali na hatarishi kwa maisha ya mtu)	Athari za kupoteza fahamu	Athari mbaya za chanjo (katika eneo la kudungwa na la kimfumo)
Kwenye Upumuaji	Upungufu wa pumzi, kupumua kunakotoa sauti kama winja/mluzi, kubanwa kwa mfumo wa upumuaji (bronchospasm), sauti ya juu ya winja/mluzi sababu ya upumuaji (stridor), kupungua kwa kiwango cha oksijeni kwenye tishu (hypoxia)	Kubadilika; ikiwa inaambatana na wasiwasi, inaweza kuwa na kiwango cha juu cha kupumua	HAIHUSIKI
Kwenye mfumo wa Moyo	Shinikizo la chini la damu, kasi ya juu ya mapigo ya moyo	Kubadilika; inaweza kuwa na shinikizo la chini la damu au kasi ya chini ya mapigo ya moyo wakati wa tukio la kupoteza fahamu	HAIHUSIKI
Tumboni	Kichefuchefu, kutapika, kubanwa tumbo, kuhara	Kichefuchefu, kutapika	Kutapika au kuharisha kunaweza kutokea
Kwenye Misuli, mifupa na vifundo	HAIHUSIKI	HAIHUSIKI	Maumivu ya misuli, maumivu ya viungo/vifundo

MAPENDEKEZO YA CHANJO

Sifa	Athari za mzio za baada ya muda mfupi (ikiwa ni pamoja na mzio mkali na hatarishi kwa maisha ya mtu)	Athari za kupoteza fahamu	Athari mbaya za chanjo (katika eneo la kudungwa na la kimfumo)
Ikiwa nitapata chanjo ya mRNA ya COVID-19 kama dozi ya kwanza, inapendekezwa nipate dozi ya pili ya chanjo ya mRNA?	Hapana	Ndiyo	Ndiyo

Watoa huduma za afya au idara za afya nchini Marekani zinaweza kutaka ushauri kutoka kwa mradi wa Tathmini ya Usalama wa Kimatibabu wa Chanjo wa COVIDvax (<https://www.cdc.gov/vaccinesafety/ensuringsafety/monitoring/cisa/index.html>) kuhusiana na swali tata la usalama wa chanjo ya COVID-19 ambalo halijashughulikiwa kwa kina na mwongozo wa CDC kuhusu mgonjwa fulani anayeishi Marekani.

Wataalam wa huduma ya afya wanapaswa kufahamu jinsi ya kutambua athari za mzio za baada ya muda mfupi, ikiwa ni pamoja na mzio mkali na hatarishi kwa maisha ya mtu, na kuwa na uwezo wa kutibu hali hizi wakati wa utoaji wa chanjo. Tiba inayofaa ya matibabu kwa athari kali za mzio lazima ipatikane baada ya muda mfupi ikiwa athari kali ya mzio mkali na hatarishi kwa maisha ya mtu wa baada ya muda mfupi itatokea kutokana na utoaji wa chanjo ya COVID-19. Angalia Usimamizi wa Mzio Mkali na Hatarishi kwa Maisha ya Mtu katika Maeneo ya Utoaji wa Chanjo za COVID-19 | CDC kwa mwongozo wa ziada. <https://www.cdc.gov/vaccines/covid-19/info-by-product/pfizer/anaphylaxis-management.html>

Upotezaji fahamu unaweza kutokea kuhusiana na chanjo za sindano, hasa miongoni mwa vijana. Taratibu zinapaswa kuwekwa ili kuzuia majeraha ya kuanguka na kudhibiti athari za upotezaji fahamu. Inapendekezwa watu wote wachunguzwe baada ya kupata chanjo ya COVID-19 kwa angalau dakika 15. Wagonjwa wanapaswa kuketi au kulala chini wakati wa uchunguzi ili kupunguza hatari ya kuimbia iwapo watazimia. Ikiwa kutakuwa na upotezaji fahamu, wagonjwa wanapaswa kuchunguzwa hadi dalili ziishe.

4. Je, umewahi kupata athari ya mzio kwa chanjo nyingine (mbali na chanjo ya COVID-19) au dawa nyingine kwa mfumo wa sindano?

Historia ya athari ya mzio ya baada ya muda mfupi (ndani ya saa 4) kwa chanjo nyingine yoyote au tiba ya sindano (yaani, chanjo za kudungwa kwenye misuli, kwenye mishipa, au za chini ya ngozi au tiba zisizohusiana na kijenzi cha chanjo za COVID-19) ni tahadhari kwa chanjo zilizo dhidi kwa sasa za COVID-19. Chanjo inaweza kutolewa, lakini unapaswa kuwashauri wagonjwa kuhusu hatari zisizojulikana za kupata athari kali ya mzio na ujadili mlingano wa hatari hizi dhidi ya manufaa ya chanjo. Kucheleweshwa/kuahirishwa kwa

chanjo na/au ushauri wa mtaalam wa kinga na mzio inaweza kuzingatwa. Uzingatiaji wa chanjo ni pamoja na kuwa katika hatari ya SARS-CoV-2, hatari ya ugonjwa mkali au kifo kutokana na COVID-19, maambukizi ya hapo awali ya COVID-19, hatari isiyojulikana ya mzio mkali na hatarishi kwa maisha ya mtu kufuatia chanjo ya COVID-19, na uwezo wa mpokeaji kupata huduma mara moja kutokana na mzio mkali na hatarishi kwa maisha ya mtu, ikiwa ni lazima. **Watu hawa wanapaswa kufuatiliwa kwa dakika 30 baada ya kupata chanjo.**

Orodha Hakikishi ya Kabla ya Chanjo za COVID-19

Maelezo kwa Wataalamu wa Huduma ya Afya



5. Mazingatio ya Kimatibabu:

Mwitikio	Uzingatiaji
Mwanamke mwenye umri wa miaka 18 hadi 49	<p>Wanawake wenye umri wa miaka 18 hadi 49 wanaweza kupokea chanjo yoyote iliyoidhinishwa na FDA ya COVID-19. Hata hivyo, wanapaswa kufahamishwa kuhusu hatari nadra lakini inayoongezeka ya ugonjwa wa kuganda damu kote mwilini (TTS) baada ya kupokea Chanjo ya Janssen ya COVID-19 www.fda.gov/emergency-preparedness-and-response/coronavirus-disease-2019-covid-19/janssen-covid-19-vaccine na upatikanaji wa chanjo zingine zilizooidhinishwa na FDA za COVID-19.</p> <p>TTS ni dalili za ugonjwa nadra ambazo zinahusisha ugonjwa mkali wa kuganda damu kwenye mishipa au ateri na mwanzo mpya wa kuwa na idadi ndogo ya chembechembe za damu kwa wagonjwa ambao hawana matumizi yanayojulikana ya hivi karibuni ya heparini.</p> <p>Nyenzo za ziada kwa mafunzo ya mgonjwa zinaweza kupatikana katika www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/safety/JJUpdate.html.</p>
Nimekuwa na athari kali ya mzio kwa kitu kingine mbali na chanjo au tiba ya sindano kama vile mizio ya vyakula, mnyama kipenzi, sumu, mazingira au dawa za kumeza	<p>Athari za mzio, ikiwa ni pamoja na athari kali za mzio, ZISIZOHUSIANA na chanjo, tiba ya sindano, au vijenzi vya chanjo ya COVID-19, SIO hali zinazoweza kuzuia usipate chanjo au tahadhari za kuchanjwa na chanjo zilizooidhinishwa kwa sasa za COVID-19. Hata hivyo, watu ambao wamekuwa na athari kali za mzio kwa kitu chochote, bila kujali sababu, wanapaswa kufuatiliwa kwa dakika 30 baada ya kupata chanjo.</p>
Nilikuwa na COVID-19 na nilitibiwa kwa kingamwili za protini zinazotengenezwa katika maabara (monokloni) au seramu ya damu kutoka kwa mtu aliyepata ahueni	<p>Chanjo inapaswa kutolewa kwa watu bila kujali historia ya maambukizi ya SARS-CoV-2 yaliyo na dalili na yasiyo na dalili. Hakuna kipindi cha chini zaidi cha muda kinachopendekezwa baina ya maambukizi na kupata chanjo.</p> <p>Hata hivyo, chanjo inapaswa kuahirishwa kwa angalau siku 90 ikiwa mgonjwa alipokea kingamwili za protini zinazotengenezwa katika maabara (monokloni) au seramu ya damu kutoka kwa mtu aliyepata ahueni kama matibabu ya COVID-19. Hii ni hatua ya tahadhari hadi wakati maelezo ya ziada yatakapopatikana, ili kuzuia uingiliaji matibabu ya kingamwili na miiitiko ya kinga inayosababishwa na chanjo.</p>

Orodha Hakikishi ya Kabla ya Chanjo za COVID-19

Maelezo kwa Wataalamu wa Huduma ya Afya



Mwitikio	Uzingatiaji
<p>Nimekuwa na dalili za ugonjwa wa kuvimba viungo vingi; aidha MIS-C (kwa watoto) au MIS-A (watu wazima)</p>	<p>Hajjulikani ikiwa watu walio na historia ya MIS-C au MIS-A wako katika hatari ya mwitikio wa kinga usioweza kudhibitiwa kutokana na chanjo ya COVID-19.</p> <p>Watu walio na historia ya MIS-C au MIS-A wanaweza kuchagua kupata chanjo. Mazingatio ya kupewa chanjo yanaweza kujumuisha:</p> <ul style="list-style-type: none"> ■ Kupona kimatibabu kutokana na MIS-C au MIS-A, ikiwa ni pamoja na kurudi kwa uendeshaji wa kawaida wa moyo ■ Hatari binafsi ya kupata COVID-19 mbaya na kali (kwa mfano, umri, matatizo yaliyopo) ■ Kiwango cha maambukizi ya COVID-19 katika jamii na hatari binafsi ya kuambukizwa tena ■ Ukosefu wa data ya usalama wa chanjo za COVID-19 kufuatia maradhi haya ■ Wakati wa matibabu yoyote ya urekebishaji wa kinga (miongozo ya jumla ya desturi bora inaweza kurejelewa kwa maelezo zaidi https://www.cdc.gov/vaccines/hcp/acip-recs/general-recs/index.html) <p>Kwa sababu ushahidi wa sasa unaonyesha kuwa hatari ya kuambukizwa tena na SARS-CoV-2 iko chini katika miezi baada ya maambukizi ya kwanza, watu walio na historia ya MIS-C au MIS-A wanapaswa kuzingatia kuchelewesha chanjo hadi watakapopona maambukizi yao na kwa siku 90 baada ya tarehe ya utambuzi wa MIS-C au MIS-A.</p> <p>Mgonjwa, mlezi (walezi) wake, na timu yake ya matibabu au mtaalam wanapaswa kuwa na mazungumzo ya pamoja ili kusaidia katika maamuzi ya chanjo ya COVID-19. Watoa huduma za afya na idara za afya wanaweza pia kuomba ushauri kutoka kwa Mradi wa Tathmini ya Usalama wa Kimatibabu wa Chanjo katika www.cdc.gov/vaccinesafety/ensuringsafety/monitoring/cisa/index.html.</p>
<p>Nina kinga dhaifu (maambukizi ya VVU, saratani)</p> <p>Ninatumia dawa au tiba zinazofubaza ukosefu kinga</p>	<p>Chanjo za COVID-19 zinaweza kutolewa kwa watu walio na matatizo yaliyopo ya kimatibabu, kama vile maambukizi ya VVU au matatizo mengine yanayoathiri kinga ya mwili, au ambao wanatumia dawa au tiba zinazofubaza ukosefu kinga, ambao hawana hali zinazowazuia wasipate chanjo.</p> <p>Hata hivyo, wanapaswa kushauriwa kuhusu maelezo yasiyoyulikana ya usalama wa chanjo na ufanisi katika idadi ya watu wasio na kinga thabiti, pamoja na uwezekano wa mwitikio uliopungua unaowezekana wa kinga na hitaji la kuendelea kufuata mwongozo wote wa sasa ili kujikinga wenyewe dhidi ya COVID-19.</p> <p>Chanjo za COVID-19 zinaweza kutolewa bila kujali matibabu ya dawa zinazopunguza uvimbe mwilini (corticosteroid), ikiwa ni pamoja na matibabu ya sehemu ya juu ya mwili au ya ndani ya viungo. Kutolewa kwa chanjo tena hakupendekezwi baada ya kupata tena uthabiti wa kinga.</p>
<p>Nina matatizo ya kuvuja damu</p> <p>Ninatumia dawa za kuzuia kuganda kwa damu</p>	<p>Kama ilivyo kwa chanjo zote, aina yoyote ya chanjo ya COVID-19 inaweza kutolewa kwa wagonjwa hawa, ikiwa daktari anayefahamu hatari ya kuvuja damu ya mgonjwa atabaini kuwa chanjo inaweza kutolewa kupitia misuli kwa usalama adilifu.</p> <p>ACIP inapendekeza mbinu ifuatayo ya chanjo ya misuli kwa wagonjwa walio na matatizo ya kuvuja damu au wanaotumia dawa za kuzuia kuganda kwa damu: Sindano nyembamba kabisa (wembamba wa 23 au ndogo zaidi) inapaswa kutumika kwa chanjo, ikifuatiwa na mgandamizo thabiti kwenye eneo lililodungwa, bila kusugua, kwa angalau dakika 2.</p> <p>Watu ambao mara kwa mara hutumia aspirini au dawa za kuzuia kuganda kwa damu kama sehemu ya dawa zao za kawaida hawahitaji kuacha dawa hizi kabla ya kupokea chanjo yoyote ya COVID-19.</p>

Orodha Hakikishi ya Kabla ya Chanjo za COVID-19

Maelezo kwa Wataalamu wa Huduma ya Afya



Mwitikio	Uzingatiji
<p>Historia ya kuwa na idadi ndogo ya chembechembe za damu inayosababishwa na heparini (HIT)</p>	<p>Ingawa kisababishi cha ugonjwa wa kuganda damu kote mwilini (TTS) unaohusishwa na Chanjo ya COVID-19 ya Janssen hakijulikani wazi, inaonekana kinafanana na ugonjwa mwingine nadra unaosababishwa na kinga, ugonjwa wa kuwa na idadi ndogo ya chembechembe za damu inayosababishwa na heparini (HIT). Hadi maelezo zaidi yatakapopatikana, wataalam wanashauri kwamba watu walio na historia ya kupata kipindi cha ugonjwa unaosababishwa na kinga ulio na sifa za kuganda damu na idadi ndogo ya chembechembe za damu, kama vile HIT, wanapaswa kupewa chanjo nyingine ya COVID-19 (yaani chanjo ya mRNA) ikiwa imekuwa siku 90 au chini tangu maradhi yao yapone. Baada ya siku 90, wagonjwa wanaweza kupewa chanjo yoyote iliyoidhinishwa na FDA ya COVID-19.</p> <p>Wataalam wanaamini kuwa sababu zifuatazo hazifanyi watu kuwa na hatari ya juu ya kupata TTS baada ya kupokea chanjo ya Janssen ya COVID-19. Watu walio na hali hizi wanaweza kupewa chanjo yoyote iliyoidhinishwa na FDA ya COVID-19, ikiwa ni pamoja na chanjo ya Janssen ya COVID-19:</p> <ul style="list-style-type: none"> ■ Historia ya awali ya ugonjwa wa kuganda damu kwenye miguu, mikono au kinena ■ Sababu za hatari ya ugonjwa wa kuganda damu kwenye miguu, mikono au kinena (kwa mfano, ukosefu wa protini za kugandisha damu (thrombophilia) unaorithi au kupata ikiwa ni pamoja na Factor V Leiden; ubadilikaji wa jeni ya protini ya ini ya 20210A; ugonjwa wa mfumo wa mwili kushambulia kimakosa protini za mwili (antiphospholipid); ukosefu wa protini C, protini S au protini inayodhibiti kuganda kwa damu (antithrombin) ■ Historia ya awali ya aina zingine za kuganda kwa damu ambazo hazihusiani na kuwa na idadi ndogo ya chembechembe za damu ■ Ujauzito, baada ya kujifungua, au kupokea dawa za kuzuia mimba unaotumia homoni (kwa mfano, mchanganyiko wa dawa za kuzuia mimba kumeza, kiraka cha homoni, pete) <p>Nyenzo za ziada kwa mafunzo ya mgonjwa zinaweza kupatikana katika www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/safety/JJUpdate.html.</p>
<p>Kwa sasa ni mjamzito au ninanyonyesha</p>	<p>Wanawake wajawazito au wanaonyonyesha wanastahiki na wanaweza kupokea chanjo yoyote iliyoidhinishwa ya COVID-19 kwa sasa.</p> <p>Kulingana na maarifa yaliyopo kwa sasa, wataalam wanaamini kuwa chanjo za COVID-19 haziwezi kuleta hatari kwa mwanamke mjamzito au kwa kijusi/kichanga. Chanjo zilizoidhinishwa na FDA za COVID-19 haziwezi kusababisha maambukizi kwa mama au kijusi/kichanga. Hata hivyo, hatari zinazowezekeka za chanjo ya COVID-19 kwa idadi hii hazijulikani kwa sababu chanjo hazijachunguzwa kwa wanawake wajawazito.</p> <p>Wakati wa kufanya uamuzi, wanawake wajawazito na watoa huduma wao wa afya wanapaswa kuzingatia kiwango cha maambukizi ya COVID-19 katika jamii, hatari binafsi ya mgonjwa kuambukizwa COVID-19, hatari zinazoongezeka za kupata maradhi makali ya COVID-19 kwa mgonjwa na hatari zinazoweza kutokea kwa kijusi/kichanga, manufaa yanayojulikana na yanayowezekeka ya chanjo, ufanisi ya chanjo, athari za chanjo, na upungufu wa data ingawa zinaongezeka kupatikana kuhusu matumizi ya chanjo wakati wa ujauzito.</p> <p>Wanawake wajawazito, wanaonyonyesha na waliojifungua wenye umri wa miaka 18 hadi 49 wanapaswa kufahamu hatari nadra ya TTS baada ya kupokea Chanjo ya Janssen ya COVID-19 na kuhusu upatikanaji wa chanjo zingine zilizoidhinishwa na FDA za COVID-19 (yaani, chanjo za mRNA).</p>
<p>Nimedungwa vijaza ngozi</p>	<p>Chanjo za COVID-19 zilizoidhinishwa na FDA zinaweza kutolewa kwa watu ambao wamepokea vijaza ngozi vya sindano na ambao hawana hali zinazowazuia wasipate chanjo au tahadhari ya kupata chanjo.</p> <p>Ingawa sio mara kwa mara, watu hawa wanaweza kupata uvimbe wa muda au karibu na eneo la kudungwa sindano ya ujazaji (kawaida kwenye uso au midomo) baada ya kupata dozi ya chanjo ya COVID-19. Watu hawa wanapaswa kushauriwa wawasiliane na mtoa huduma wao wa afya ikiwa watapata uvimbe katika au karibu na eneo la vijaza ngozi baada ya kupewa chanjo.</p>